MIAKA 62 YA UHURU

# Viongozi 26 wapya kuanika mali zao Maadili

Na Zena Chande

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeongeza viongozi 26 katika orodha ya viongozi wanaotambulika kwa mujibu wa sheria, na hivyo kufanya viongozi wanaotambulika sasa kufikia 62.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa kitengo cha mawasiliano serikalini ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Honoratus Ishengoma, alisema mabadiliko hayo yamefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa mujibu wa kifungu cha 4 (2) cha sheria ya maadili inayompa mamlaka ya kuongeza, kufuta au kuboresha orodha ya viongozi wanaotambulika kwa mujibu wa sheria.

"Kuna tangazo tumetoa kwenye gazeti la HabariLEO (gazeti hili, jana), hivyo viongozi waliotangazwa wanatakiwa kuwajibika kwa kufuata masharti yote yaliyomo kwenye sheria za maadili ya umma tangu tarehe ya tangazo hilo… nyadhifa zao ni nyeti wanastahili kutambuliwa kama viongozi wa umma," alisema.

Orodha mpya ni Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mkaguzi Mkuu wa Nje, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya.



Wengine ni Kamanda wa Usalama Barabarani Mkoa na Wilaya, Mkuu wa Magereza Mkoa na Mkuu wa Gereza, Ofisa katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuanzia cheo cha Kamishna Msaidizi, Ofisa katika Idara ya Uhamiaji kuanzia cheo cha Kamishna Msaidizi.

Pia, Msajili, Mrajisi, Naibu Msajili, Naibu Mrajisi, Msajili Msaidizi, Mrajisi Msaidizi, katika Wizara, Idara za Serikali, Taasisi, Shirika, Wakala wa Serikali, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Aidha, wapo Ofisa kuanzia cheo cha Kamishna Msaidizi, katika wizara, Idara ya Serikali, Taasisi, Shirika la Umma, Mamlaka na Wakala wa Serikali,

Naibu Karani wa Baraza la Mawaziri, Mfamasia Mkuu wa Serikali, Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Msaidizi.

Wengine ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kanda, Mkoa, na Wilaya, Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkuu wa Mashtaka wa Mkoa, Mwendesha Mashtaka wa Wilaya, Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Kabidhi Wasii Mkuu, Ofisa Madini Mkazi, Msuluhishi na Muamuzi katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

Alitaja viongozi wengine kuwa ni Mwenyekiti na Mjumbe katika Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Wadhamini au Bodi ya Ushauri ya Wizara, Mpiga Picha wa Rais, Naibu Mnikulu, Katibu Msaidizi binafsi wa Rais, Mkuu wa Takukuru wa Mkoa na Mkuu wa Takukuru wa Wilaya, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Mtendaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu, Wakili Mkuu wa Serikali na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali.

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilifanya marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 13 ya mwaka 1995 kwa lengo la kuboresha kifungu cha 4 chenye orodha ya Viongozi wanaowajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa umma.

Kwa mujibu wa Sekretarieti hiyo, dhumuni kubwa la kubadili sheria hiyo ni baada ya kubaini kuwa wapo watumishi kutoka Taasisi mbalimbali za Umma na binafsi ambao ni Viongozi lakini hawajatajwa na Sheria hiyo jambo linalowafanya kutohusika kabisa na sheria hiyo

Kwa mujibu wa sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Viongozi wote wa Umma wanatakiwa kujaza Fomu ya Tamko la Mali na Madeni na kuiwasilisha kwa Mwenyekiti wa Tume si zaidi ya Desemba 31, mwaka 2021.